# Wafugaji, wafanyabiashara walia ukosefu wa viwanda

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAFUGAJI na wafanyabiashara wa mazao ya mifugo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wamelalamikia ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao hayo hali inayosababisha kukosa fursa ya masoko na nje ambayo yana tija zaidi kuliko ya ndani.

Wadau hao wamedai kuwa mikoa hiyo ni miongoni mwa maeneo nchini yenye mifugo mingi lakini haina tija nzuri kutokana na kukosekana kwa viwanda hivyo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti waliiomba serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kujenga viwanda ama kualika wawekezaji kutoka nje wanaoweza kuwekeza kwenye viwanda hivyo ili kuwasogezea soko.

Mmoja wa wadau hao, Aloyce Shija ambaye ni mfugaji na mfanyabiashara wa mifugo, alisema wamekuwa wakizalisha ngozi na mazao mengine ya mifugo lakini mengi yanatupwa kwa sababu hakuna viwanda vya kuyaongeza thamani.

Alisema hali hiyo inawafanya kutopata faida kubwa kama ilivyo kwenye mazao mengine yakiwamo ya kilimo kwa maelezo kuwa sehemu kubwa ya mazao hutupwa.

**Sasa kama kungekuwapo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo Uwanja wa Ndege Songwe ingekuwa ni fursa kubwa kwa wananchi, uwekezaji ni mkubwa lakini bidhaa za kusafirisha hakuna na wanufaika wakubwa ni wageni.**

"Ukiangalia katika maeneo mengi ya mikoa hii, mifugo ni mingi sana, ukienda maeneo kama Chunya, Mbarali, Momba, Sumbawanga na Songwe huko kuna mifugo mingi lakini tunachouza ni nyama na maziwa, lakini kuna mazao mengine soko halipo," alisema Shija.

Alisema katika mataifa mengine mifugo ikichinjwa yapo mazao yanahitajika viwandani kama kwato, pembe na ngozi ambayo yanahitajika viwandani kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zingine.

Alisema asilimia kubwa ya mazao hayo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yanatupwa kwa sababu havipo viwanda vya kuyachakata ili yapelekwe kwenye masoko.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali inapoteza mapato ambayo yangepatikana kutokana na usafirishaji wa mazao hayo ya mifugo kupitia masoko mbalimbali.

Mfanyabiashara wa ng'ombe katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo, Joel Amos alisema kutokana na mahitaji makubwa ya nyama nje ya nchi serikali inapaswa kutengeneza fursa ambazo zitasaidia uchakataji wa mazao hayo.

Alisema katika mikoa hiyo kuna kila aina ya njia za usafirishaji ambazo zingetumika kusafirisha mazao hayo ukiwamo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

"Sasa kama kungekuwapo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo Uwanja wa Ndege Songwe ingekuwa ni fursa kubwa kwa wananchi, uwekezaji ni mkubwa lakini bidhaa za kusafirisha hakuna na wanufaika wakubwa ni wageni," alisema Amos.

Ofisa Mifugo kutoka katika Bodi ya Nyama Tanzania (TBM) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Mpoki Alinanuswe, alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kwamba kwa kanda hiyo kuna kiwanda kimoja pekee.

Alisema kwa sasa kanda hiyo wafugaji wamekuwa wakifuga kisasa na kuzingatia kanuni za ufugaji kibiashara lakini tatizo ni namna ya kuyafikia masoko ya nje ya nchi.

Alisema kupitia sekta ya mifugo wamekuwa wakihamasisha ufugaji wa kibiashara na kuongeza thamani ya ng'ombe sambamba na utunzaji wa chakula cha kutosha katika msimu wa mavuno ya mazao ili wauze kwa bei nzuri.

CamScanner